


SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



Kusimama Juu ya Mabega ya Muindaji



Nyota iliyopo katikati ya picha inaitwa Betelgeuse, ipatikanayo katika mabega ya muindaji mkubwa katika konstilesheni ya Orion. Konstilesheni ni picha katika anga la usiku katika maumbo mbali mbali ya vitu, wanyama na watu ambazo zimetengenezwa kwa kuunganisha nyota, kama fumbo la kuunganisha nukta ili kupata umbali Orion inaweza kuonekana kwa urahisi kua kutumia macho, na huonekana katika kizio cha kaskazini wakati wa baridi. Betelgeuse ni nyota yenye rangi ya Chungwa iliyopo upande wa juu kushoto kwa nyota tatu maarufu zinazotengeneza mkanda wa muindaji. Unaweza kutoka nje usiku wa leo ili kujionea mwenyewe!

Katika picha hii, Betelgeuse inaweza kuonekana ni ndogo lakini ni Red Supergiant yenye ukubwa karibu mara 1000 zaidi ya Jua letu na inang'aa mara 100,000 zaidi! Lakini muonekano wake huu wa kupendeza una għarama zake pia. Betelgeuse inakaribha kufa, tena kifo cha milipuko mkubwa na wenze nguvu uitwao Supernova. Anġalia pichani, unawēza kuona imeshaanza kupoteza baadhi ya maada zake katika tabaka lá nje!

Kama ilivyo kwa Jua, Betelgeuse ilikuwa ni nyota ya kawaida tu. Ila imezeeka kuvimba na kuwa kubwa, hivyo kuanza kushindwa kuhimili matabaka yake ya nje na kutawanya maada zake huko angani. Maada ambazo zimetengeneza nusu duara, ambalo unawēza kuliona katika picha likiwa limejikunja katika upande wa kushoto wa nyota.

Ukiweza kuangalia kwa ukaribu, unawēza kuona pia kitu cha kushangaza, mstari ulionyooka wa maada katika upande wa kushoto wa picha. Wanasyansi wanaamini kuwa mstari huu hauna uhusiano wowote na nyota. Unaonekana kama ni ukingo wa wingu jeusi la vumbi na gesi ambalo limemulikwa na mwanga wa Betelgeuse. Kama wanachofikiria ni sawa, inaonekana kuwa Betelgeuse inaelekeea kugongħana mda si mrefu!

COOL FACT

Ukilinganisha na umbali wa angani nyota ya Betelgeuse ipo karibu sana na Dunia. Hii inamaanisha kuwa ikilipuka katika supernova, itaonekana vizuri sana kwani itawaka kama mwezi unavyowaka angani!



More information about EU-UNAWE
Space Scoop: www.eu-unawe.org/kids/